

Swahili/norsk

Ukweli kuhusu VUKIBI na UKIMWI

Fakta om hiv og aids

Aids er en alvorlig sykdom som siden begynnelsen av 1980-tallet har spredd seg over hele verden. Aids skyldes et virus, hiv, som overføres fra person til person i bestemte situasjoner.

Hva er hiv?

Hiv er forkortelse for humant immunsvikt virus. Personer med hiv vil vanligvis ikke føle seg syke de første årene etter at de er smittet, men viruset vil etterhvert bryte ned kroppens motstandskraft mot smittestoffer.

Personer som har fått hiv vil ha viruset i kroppen og kunne smitte andre resten av livet.

Hva er aids?

Det alvorligste stadium i sykdomsutviklingen kalles aids. Aids er forkortelse for acquired immune deficiency syndrom. En person med hiv utvikler aids når kroppens motstandskraft er så svekket at den ikke lenger klarer å uskadeliggjøre smittestoffer som virus, bakterier og sopp. Personer med hiv vil etter hvert utvikle aids hvis de ikke får behandling. Vanligvis tar det 8-10 år fra man blir smittet til man utvikler aids.

I noen deler av verden er aids en av de vanligste dødsårsakene. Gjennomsnittlig levealder har derfor i noen land gått ned med ca. 10 år.

UKIMWI ni ugonjwa mbaya ambao umetapakaa kote duniani tangu mwanzoni mwa miaka ya 1980. UKIMWI husababishwa na virusi moja iitwayo VUKIBI, ambayo huenezwa kupitia mtu mmoja hadi mwingine, wakati wakiwa katika hali na vitendo fulani.

VUKIBI ni kitu gani?

VUKIBI ni ufupisho wa virusi ya upungufu wa kinga katika binadamu. Neno hili (VUKIBI), litatumika hapa kama ni tafsiri ya HIV ("humant immunsvikt virus", kwa Kinorway, na "human immunodeficiency virus", kwa Kiingereza). Watu wenye VUKIBI, kwa kawaida hawajihisi wagonjwa miaka ya awali baada ya kuambukizwa. Lakini virusi hiyo, baada ya kipindi, huvunja nguvu ya mwili dhidi ya viini vya maabukizo. Watu waliopata VUKIBI, huishi na virusi hiyo mwilini na kuweza kuwaambukiza wengine kwa miaka yote iliyobaki katika maisha yao.

UKIMWI ni kitu gani?

Ile hali mbaya kabisa katika maendeleo ya maradhi huitwa UKIMWI. UKIMWI ni ufupisho wa ukosefu wa kinga mwilini. Mtu mwenye VUKIBI hatimaye hupata UKIMWI, wakati nguvu ya mwili kujihami dhidi ya magonjwa inadhoofika, na mwili unashindwa tena kujikinga dhidi ya viini vya maambukizo kama vile virusi, vijasumu (bakteria) na kuvu. Watu wenye VUKIBI, baada ya muda, hupata UKIMWI, ikiwa hawashughulikiwi na kupatiwa matibabu. Kwa kawaida huchukua muda wa miaka 8 hadi 10, kutoka pale mtu anapoambukizwa hadi apatapo UKIMWI. Katika sehemu fulani za dunia, UKIMWI ni sababu ya kawaida kabisa ya vifo. Katika nchi fulani, kwa hivyo, urefu wa wastani wa maisha, umeshuka kwa miaka 10.

Hvordan smitter hiv?

Hiv smitter:

1. Ved ubeskyttet samleie mellom kvinne og mann eller mellom menn. Hvem som helst kan få hiv ved ubeskyttet samleie med en person som har viruset. Årsaken til smitte er direkte kontakt med viruset som finnes i blod, sæd eller skjedesekret.

Hiv kan overføres fra mann til kvinne, fra kvinne til mann og fra mann til mann. Hiv smitter lettere hvis en eller begge parter har andre seksuelt overførbare sykdommer (SOS). Det kan også være en risiko for overføring av virus gjennom munnsex, det vil si kontakt mellom kjønnsorganer og munn/tunge. Dette er spesielt aktuelt hvis det finnes rifter eller sår i munnen eller på kjønnsorganene.

2. Ved bruk av sprøyter og sprøytespisser forurenset med hiv.

3. Ved blodoverføring dersom blodet inneholder hiv.

4. Fra mor til barn under svangerskapet, fødselen eller ved amming.

Jinsi VUKIBI inavyoambukiza

VUKIBI huambukiza kama ifuatavyo:

1. Kwa kujamiiana baina mwanamke na mwanamume, au baina wanaume, bila kutumia zana ya kinga, yaani mpira wa uume (kondomu). Ye yote yule aweza kupata VUKIBI kwa kujamiiana na mtu aliye na virusi hiyo, pasipo na matumizi ya mpira wa uume. Sababu ya ambukizo ikiwa mgusano bila kinga baina ngozi za tupu (dhakari, uke, mkundu). Hapo mtu hukabilishwa na virusi iliyomo katika damu, shahawa au utoko wa uke.

VUKIBI huambukiza kupitia mwanamume hadi mwanamke, kupitia mwanamke hadi mwanamume, na kupitia mwanamume hadi mwanamume. VUKIBI huambukiza kwa urahisi zaidi ikiwa mmoja au wote wawili wanaoshiriki katika ngono wana magonjwa mengine ambayo yanaweza kuambukiza kwa njia ya ngono. Vile vile, hatari ya kueneza virusi inaweza kutokea katika ”ngono ya mdomo”, yaani kugusana kwa tupu (dhakari, uke, mkundu) na mdomo au ulimi. Hatari hii huzidi wakati kuna michubuko au vijidonda mdomoni au kwenye tupu.

2. Kwa kutumia sindano na ncha za sindano ambazo zimechafuliwa na VUKIBI.

3. Kwa kupandishwa damu wakati damu ile ikiwa ina VUKIBI.

4. Kwa kupitia mama hadi mtoto wakati wa ujauzito, hali kadhalika wakati wa kujifungua au wakati wa kunyonyesha.

Hvordan unngå smitte?

Det eneste effektive beskyttelsesmiddel mot hiv er kondom. Kondom beskytter også mot andre seksuelt overførbare sykdommer som herpes, klamydia, gonore og mot uønsket graviditet. Også ved munnsex bør man bruke kondom.

P-piller og spiral beskytter bare mot uønsket graviditet

Injiserende stoffbrukere må unngå å dele sprøyter med andre. Velger man likevel å dele sprøyteutstyr, må sprøyte og sprøytespiss rengjøres grundig med klorin mellom hver injeksjon på følgende måte:

Skyll gjennom utstyret med lunkent vann 5 ganger.

Trekk klorin opp i spiss og sprøyte. La klorinen stå i utstyret i minst 5 minutter.

Skyll gjennom utstyret med lunkent vann 5 ganger.

Medisinsk behandling av gravide med hiv har redusert risikoen for smitte fra mor til barn betydelig. For å unngå at barnet får hiv er det viktig at moren får regelmessig medisinsk oppfølging.

Jinsi ya kuepukana na ambukizo

Njia pekee ya kujikinga na VUKIBI ni matumizi ya mpira wa uume (kondomu). Mpira wa uume vile vile huhami dhidi ya magonjwa mengine yanayoambukiza kwa njia ya ngono, kama vile "herpes"(kwa Kinorway na Kiingereza), yaani ugonjwa fulani wa kutoka malengenge ngozini; "klamydia"/"Chlamydia" (kwa Kinorway na Kiingereza), yaani maradhi fulani yanayoenezwa kwa njia ya ngono na vijidudu vya aina Chlamydia, ambavyo vinalingana na vijasumu na virusi; na kisonono. Mpira wa uume vile vile husaidia kama kinga dhidi ya utungaji wa mimba. Yapasa pia kutumia mpira wakati wa ngono ya mdomo.

Matumizi ya zana zifuatazo huzuia mimba tu: 1.vidonge vya kuzuia mimba 2. "spiral" (kwa Kinorway) au "IUCD" (intrauterine contraceptive device) (kwa Kiingereza), yaani aina ya kijitanzi/kijidude kipitishwacho shingo ya mji wa uzazi na kuwekwa katika mji wa uzazi.

Watumiaji wa madawa levyaji kwa kutumia sindano, wajihadhari na waekuepukane na kutumia sindano kijumuiya.

Ikiwa watumiaji hao wameamua kutumia sindano kijumuiya, basi wahakikishe sindano na ncha za sindano zimesafishwa vizuri kwa kutumia klorini kila baada ya kudunga, kwa kufuata utaratibu ufuatao:

Suiza zana mara 5 kwa kutumia maji fufutende (yalio moto kiasi) Vuta klorini kwenye sindano kupitia ncha ya sindano. Iache klorini ibaki humo kwa muda usiopungua dakika 5.

Baada ya hapo suiza zana mara 5 kwa kutumia maji fufutende (yalio moto kiasi).

Kufanyiwa matibabu wajawazito wenye VUKIBI imepunguza mno hatari ya mama kumwambukiza mtoto. Ili kuepukana na kumwambukiza mtoto VUKIBI, ni muhimu kwa mama kupata kupimwa na kuchunguzwa kimatibabu kwa utaratibu maalumu wa mara kwa mara.

Hiv smitter ikke

Ved vanlig sosial omgang.
Gjennom hel hud.
Gjennom luft og vann.
Gjennom mat og drikke.
Via spisebestikk, servise og lignende.
Via sengetøy, håndklær og lignende.
Via toalettseter og badebasseng.
Ved kyssing.
Ved nysing og hoste.
Gjennom svette.
Gjennom snørr og tårer.

Sterile sprøyter som brukes på sykehus, hos legen og på helsestasjoner medfører ingen fare for overføring av hiv eller andre sykdommer som smitter gjennom blod. Derfor er det heller ingen risiko ved å gi blod.

I Norge har vi begrensninger på hvem som får gi blod. Begrensningene gjelder blant annet menn som har sex med menn, injiserende stoffbrukere, personer som har oppholdt seg lenge eller er født i noen land utenfor Nord-Europa.

VUKIBI haiambukizi:

Kwa kukutana kijamii (yaani kuwa na mazoea na wenzako).

Kwa mgusano wa ngozi nzima (ambayo haijararuka au kuchanika).

Kwa njia ya kupitia hewa tunayopumua na maji.

Kwa kupitia maakuli na vinywaji/vitu vya kunywa.

Kwa kupitia visu, nyuma, vijiko na vyombo vya kulia, na vinginevyo kama hivyo.

Kwa kupitia matandiko, taulo za mikono au za mwili, na vinginevyo kama hivyo.

Kwa kutumia (kukalia) vitako vya vyoo (vya kiulaya) na kutumia mabwawa ya kuogelea.

Kwa njia ya kubusu mwenzako.

Kwa njia ya kuenda chafya na kukohoa.

Kwa kupitia jasho.

Kwa kupitia gole/kamasi na machozi.

Sindano zilizo muma/safi zinazotumiwa mahospitalini, kwa daktari, au kwenye vituo vya afya, hazina hatari ya kueneza VUKIBI au maradhi mengine ambayo huambukiza kupitia damu. Hali kadhalika hamna hatari ya ambukizo kwa mtu ambaye anajitolea damu kwa kuwasaidia wagonjwa wanaohitaji damu.

Katika Norway kuna viziwi vinavyohusu wale wasioweza kujitolea damu kuwasaidia wagonjwa.

Miongoni mwa wale wanaozuiliwa kujitolea damu ni wanaume wanaojamiiana na wanaume wenzao, watumiaji wa madawa levyaji kwa kudunga sindano, watu ambao wameishi muda mrefu au wamezaliwa katika nchi fulani zilizo nje ya Ulaya ya Kaskazini.

Behandling

Det finnes ingen vaksine mot hiv som beskytter mot smitte. Det finnes heller ikke medisiner som fjerner viruset fra kroppen.

Det finnes medisiner som kan hemme formeringen av viruset i blodet. Når det er små mengder virus i kroppen tar det lengre tid å svekke kroppens motstandskraft. Kroppens motstandskraft kalles immunforsvar, og ved bruk av medisiner tar nedbrytingen av immunforsvaret lengre tid. Behandlingen så langt har gitt positive resultater.

Bruken av disse medisinene krever regelmessig oppfølging hos lege. Det er viktig at hiv blir oppdaget så tidlig som mulig slik at behandling med de rette medisiner kan begynne straks det er nødvendig.

Hvis det har oppstått infeksjoner p.g.a. et svekket immunforsvar finnes det medisiner til behandling av mange av disse infeksjonene.

Personer med hiv vil få oppfølging og råd av helsetjenesten og behandling av eksperter på hivinfeksjon.

Når det gjelder medisiner og levesett som vil virke inn på sykdommen er det viktig at den som har hiv samarbeider med de som har erfaring og kunnskap om behandling . Med godt samarbeid mellom pasient og behandler er det store muligheter for at en med hivinfeksjon kan leve som frisk i mange år.

Matibabu

Haipatikani dawa ya chanjo ya VUKIBI ambayo humkinga mtu dhidi ya ambukizo. Wala hakuna madawa ambayo huondoa virusi mwilini.

Yanapatikana madawa yanayoweza kuzuia kuzaliana kwa virusi katika damu. Wakati kuna virusi chache tu mwilini, huchukua muda mrefu zaidi kudhoofisha nguvu kinzi ya mwili. Nguvu kinzi ya mwili huitwa kingamaradhi, na matumizi ya madawa husaidia kupunguza kasi ya virusi kuteketeza kingamaradhi, yaani huchukua muda mrefu zaidi kuvunja kingamaradhi. Kwa mpaka hii leo, matibabu kama haya yameleta matokeo yanayoridhisha.

Matumizi ya madawa haya yanamhitaji mgonjwa apimwe na kuchunguzwa kimatibabu kwa utaratibu maalumu wa mara kwa mara. Ni muhimu kwamba VUKIBI igunduliwe mapema iwezekanavyo, ili matibabu kutumia madawa yanayofaa yaanzwe mara tu inapohitajika.

Ikiwa kumetokea maambukizo fulani kwa sababu ya kudhoofishwa kwa kingamaradhi, basi pia yanapatikana madawa ya kutibu maambukizo mengi kati ya hayo.

Watu wenye VUKIBI huendelea kupata uchunguzi au upelelezi, pamoja na kupewa shauri na watumishi wa huduma za afya, na huendelea kupata matibabu kwa wataalamu wa maambukizo ya VUKIBI.

Inapohusu madawa, na jinsi mtu anavyoishi maisha yake, ambapo hiyo inaweza kuathiri mgonjwa, ni muhimu kwa mgonjwa huyo wa VUKIBI kushirikiana na wale ambao wana uzoefu na ujuzi wa kutibu. Ushirikiano mzuri baina ya mgonjwa na tabibu kunampa uwezekano mkubwa mwenye ambukizo la VUKIBI kujiishia miaka mingi katika afya njema.

Hivtest

Smitte med hiv fører til at kroppen danner angrepsstoffer, såkalte antistoffer for å ødelegge viruset. En hivtest tas som en blodprøve i armen. Den viser om det finnes hiv antistoffer i blodet. Man kan finne antistoffer i blodet tre til seks uker etter smitte. Det tar ca. en uke å få svar på hivtesten. På enkelte steder er det også mulig å ta en hurtigtest hvor man får resultatet etter 20 minutter. Man kan velge å være anonym når man tar en hivtest.

Det er bare hivtesten som kan gi svar på om man er smittet. Alle som tror de har vært i en risikosituasjon bør derfor teste seg. Testen er gratis og kan tas hos hvilken som helst lege. Legen skal ikke gi opplysninger om testresultat til andre uten samtykke fra den det gjelder. Dette gjelder så lenge den smittede ikke utsetter andre for smittefare.

Hivtesten er frivillig. Det betyr at ingen kan testes mot sin vilje, og alle som testes skal være informert om hva testen innebærer. Gravide får tilbud om test i forbindelse med svangerskapskontroll. Det stilles ikke krav om hivtest i forbindelse med søknad om oppholdstillatelse i Norge. Avgjørelsen i slike søknader skal ikke være knyttet til hivtesten.

Upimaji wa VUKIBI

Ambukizo la VUKIBI linafanya mwili kujenga pingamizi ambayo hujulikana kama kingamwili au zindiko, ili kuangamiza virusi. VUKIBI hupimwa kwa kutoa damu mkononi. Damu huonyesha kama inayo kingamwili ya VUKIBI. Kingamwili hujidhihirisha kwenye damu majuma matatu mpaka sita baada ya ambukizo. Huchukua muda wa juma moja kupata jibu juu ya upimaji huo. Mahali pengine unaweza kupimisha damu na kupata majibu haraka, yaani baada ya kama dakika ishirini hivi. Mtu asiyetaka kujitambulisha pia anaweza kupimisha VUKIBI.

Ni upimaji wa VUKIBI pekee ambao hutambulisha kama fulani ameambukizwa. Kwa hivyo wote wale ambao wanaamini kwamba wamewahi kujikabilisha na hali ya hatari ya maambukizo, wanasisitizwa kupimisha damu. Upimaji ni bure, na unaweza kujipimisha kwa daktari ye yote yule. Daktari haruhusiwi kutoa habari zo zote kuhusu matokeo ya upimaji huo kwa wengine, bila ya kibali cha aliyehusika. Haki hii ya siri anayo aliyeambukizwa, isipokuwa pale ambapo kuna hatari ya kwamba jamaa huyo huenda akaambukiza wengine.

Upimaji wa VUKIBI ni jambo la hiari. Hii inamaanisha kwamba hapana anayeweza kulazimishwa kupimwa, na wote wanaopimwa inapasa waarifiwe upimaji huo unamaanisha nini hasa. Wajawazito wanapewa nafasi ya kujipimisha wakati wanapopimwa mimba. Hakuna matakwa au lazima ya kujipimisha damu kwa yule ambaye anapeleka maombi ya kibali cha kuruhusiwa kuishi nchini Norway. Maamuzi ya maombi kama hayo hayafungamanishwi na lazima ya kupimwa VUKIBI.

Når hivtesten er negativ

En negativ hivtest betyr at det ikke kan påvises antistoffer i blodet. Sannsynligvis er du ikke smittet. Men kroppen trenger tid for å danne antistoffer etter at smitten har funnet sted. Bli testen tatt før antistoffene er dannet vil det gi et negativ resultat selv om viruset er i kroppen. Hvis du vet at du har utsatt deg for smitte de siste tre månedene bør du ta en ny test etter 6-8 uker.

Er du smittet uten at det ennå er dannet antistoffer kan du smitte andre.

Husk at et negativt resultat ikke betyr at du ikke kan bli smittet i fremtiden. Unngå derfor risikoadferd som ubeskyttet sex og deling av sprøyter.

Wakati upimaji wa VUKIBI waonyesha matokeo hasi.

Matokeo hasi ya upimaji wa VUKIBI inamaanisha haikubainishwa kuna kingamwili au zindiko katika damu. Yamkini hujaambukizwa. Lakini kumbuka ya kuwa mwili huhitaji muda ili kujenga kingamwili/zindiko baada ya ambukizo kutokea. Ikiwa upimaji utafanywa kabla kujengeka kwa kingamwili/zindiko mwilini, basi matokeo yatakuwa hasi ijapokuwa imo virusi mwilini. Ikiwa wajua kwamba umewahi kujikabilisha na hatari ya ambukizo miezi mitatu ya nyuma, inabidi ujipimishe upya baada ya muda wa majuma 6 hadi 8.

Kama umeambukizwa, na ijapokuwa bado kingamwili haijajidhirisha mwilini, unaweza ukaambukiza wenzio.

Kumbuka ya kwamba matokeo hasi haimaanishi kwamba huwezi kuambukizwa siku za mbele. Epukana kwa hivyo na mwendo unaohatarisha, kama vile kujamiiana bila ya kinga ya mpira wa uume, na matumizi ya sindano kijumuiya.

Når hivtesten er positiv

En positiv hivtest betyr at en er smittet og dermed kan smitte andre. Selv om kroppen danner antistoffer klarer de ikke å uskadeliggjøre viruset.

Når man får vite at man har en alvorlig smittsom sykdom vil det for de fleste melde seg mange spørsmål.

Når hivtesten er positiv blir man henvist til leger og sykepleiere som er spesialister på hiv og aids. Her vil du få svar på de spørsmålene du har, og de vil kunne gi deg råd for hvordan du kan planlegge livet ditt.

De aller fleste kan jobbe eller studere som de gjorde før de fikk vite at de var hivpositive, og det er kun på enkelte områder i livet det er nødvendig å gjøre forandringer. De største forandringene vil være at man alltid må ta hensyn risikoen det er for å smitte andre. Man må også forholde seg til helsevesenet på en måte som er ny for de fleste. Faste besøk og nært samarbeid med legen er viktig.

Wakati upimaji wa VUKIBI waonyesha matokeo chanya

Matokeo chanya ya VUKIBI inamaanisha kwamba umeshaambukizwa, na kwamba waweza kuambukiza wengine. Ijapokuwa mwili umo katika shughuli ya kujenga kingamwili, hiyo haimudu kuvunja nguvu ya virusi.

Mtu anapotambulishwa kuwa ana ugonjwa wa kuambukiza ulio mbaya, kwa wengi taarifa hii huwakabili na maswali mengi.

Wakati upimaji wa VUKIBI waonyesha matokeo chanya, aliyesibiwa hupelekwa kwa madaktari na wauguzi ambao ni wataalamu wa VUKIBI na UKIMWI. Kwa wataalamu hawa unaweza kujipatia majibu ya maswali uliyo nayo, na hao pia watakupa mashauri juu ya jinsi ya kujirekebisha na kupanga maisha yako, yaani jinsi utakavyoishi (kwa sababu ya maradhi).

Wengi kati waliosibiwa wanaweza kuendelea na kazi au kuendelea na masomo kama walivyokuwa wakifanya hapo awali, kabla ya kujua kwamba matokeo yao ya VUKIBI ni chanya. Na kuna baadhi (vitendo na hali) fulani tu za maisha ambapo yatakiwa kufanya marekebisho. Marekebisho makubwa ni kwamba mtu yambidi ajihadhari na hatari iliyopo ya kuwaambukiza wengine. Vile vile yambidi mtu kuingia katika uhusiano maalumu na huduma za afya, uhusiano ulio mpya kwa wengi. Kufika kwa daktari kwa utaratibu maalumu wa mara kwa mara, ili kuhudumiwa kimatibabu, na kuwa na ushirikiano mzuri na daktari, ni muhimu.

Ordliste

Immunforsvar

Kroppens eget forsvar mot bakterier, virus og sopp. Immunforsvaret skal hindre at vi blir syke av alle smittestoffene vi kommer i kontakt med.

Smittestoffer

Bakterier, virus eller sopp som kan lage sykdommer. Smittestoffene kommer inn i kroppen gjennom luften vi puster, gjennom det vi drikker og spiser eller gjennom seksuell kontakt og gjennom blod.

Virus

Smittestoff som trenger kroppens levende celler for å kunne formere seg.

Bakterier

Smittestoff som kan gi sykdom hos mennesker. De fleste sykdommer som skyldes bakterier kan behandles med antibiotika.

Sopp

Smittestoff som kan gi sykdommer, spesielt hos mennesker med dårlig immunforsvar.

Infeksjon

Sykdom fremkalt av bakterier, virus eller sopp.

Antistoffer

Stoffer som kroppen lager for å uskadeliggjøre smittestoffer som kommer inn i kroppen. Kroppen lager egne antistoffer for hvert enkelt av de ulike smittestoffene. For eksempel lager kroppen sitt eget antistoff mot hiv.

Msamiati

Kingamaradhi

Nguvu kinzi ya mwili dhidi ya vijasumu (bakteria), virusi na kuvu. Kingamaradhi huzuia mtu kuwa mgonjwa anapokabiliwa na viini vyote vya maambukizo.

Viini vya maambukizo

Vijasumu (bakteria), virusi au kuvu, ambavyo huleta magonjwa. Viini vya maambukizo hivi huingia mwilini kupitia hewa tunayopumua, kupitia tunachokunywa na kula, au kupitia njia ya ngono na damu.

Virusi

Kiini cha maambukizo ambacho huhitaji chembe hai au seli zilizo hai za mwili, ili kuweza kuzaliana.

Vijasumu (bakteria)

Kiini cha maambukizo ambacho huweza kuleta maradhi kwa binadamu. Magonjwa mengi yanayosababishwa na vijasumu hutibiwa na viuavijasumu ("antibiotika", kwa Kinorway, "antibiotics" kwa Kiingereza).

Kuvu

Kiini cha maambukizo ambacho huweza kusababisha maradhi, hasa kwa watu ambao hawana kingamaradhi madhubuti.

Ambukizo

Maradhi yanayosababishwa na vijasumu (bakteria), virusi au kuvu.

Kingamwili au zindiko

Mata ambazo mwili huunda ili kupiga vita na kuvunja viini vya maambukizo vinavyoingia mwilini. Mwili hujenga kingamwili maalumu kwa viini vya maambukizo mbali mbali. Kwa mfano mwili hujenga kingamwili maalumu dhidi ya VUKIBI.

”Ukweli kuhusu VUKIBI na UKIMWI”
Imetolewa na ”Statens institutt for folkehelse”
(Taasisi ya taifa ya afya ya wananchi)
ikishirikiana na ”Statens helsetilsyn”
(Ofisi ya usimamizi wa taifa wa afya).
Toleo jipya lililorudiwa na kusahihishwa 2001

"Fakta om hiv og aids"
Utgitt av Statens institutt for folkehelse
i samarbeid med Statens helsetilsyn.
Ny revideret utgave 2001

Informasjonstelefonen om aids: 810 03 200



Postboks 4404 Nydalen
N-0403 Oslo, Norway
Internett: www.folkehelse.no



Statens helsetilsyn

Trykksakbestilling:
Tlf.: 22 24 88 86 - Faks: 22 24 95 90
E-post: trykksak@helsetilsynet.dep.no
Internett: www.helsetilsynet.no